JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI LONGIDO

S.L.P. 8530, NAMANGA-ARUSHA. **SIMU Na.** 027-2539218: **E-Mail:** longido.secondary@yahoo.co.uk

Kumb.Na. LSS/ADSEC.........................................

Ndugu Mzazi/Mlezi wa: ................................... **Tarehe: 30/03/2022**

## YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA ELIMU YA SEKONDARI:

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga **Kidato cha Tano-2022** katika shule ya Sekondari Longido iliyopo mkoani Arusha. Kwa niaba ya Bodi ya shule pamoja na watumishi wote wa shule ninakupongeza wewe pamoja na mwanao, Hongera sana!

Shule ipo kilometa 79 kutoka Arusha Mjini. Usafiri wa kutoka Arusha mjini hadi Longido ni Hiace na Noah. Ukifika kituo kikuu cha mabasi Arusha, panda gari (Hiace au Noah) la Longido au Namanga mwambie dereva akushushe stand ya Longido. Kutoka hapo shule ipo umbali wa kilometa 1. Hivyo unaweza kutumia usafiri wa Tax au pikipiki ili kufika shuleni.

### A: UTARATIBU WA KUJIUNGA NA SHULE:

1. Shule itafunguliwa Tarehe .................. siku ambayo masomo yataanza rasmi. Siyo busara mwanao kuchelewa kufika shuleni bila sababu za msingi kwani unaweza kupoteza nafasi ya mwanao baada ya wiki moja kupita.
2. Shule hii ni ya Bweni, hivyo kulipa **ADA** na **michango mingine** ya shule ni lazima.
3. Mwanao hana budi kufuata sheria/taratibu/kanuni za shule ambazo zimeainishwa katika fomu hii ya kujiunga na shule. Kutozifuata sheria/taratibu/kanuni za shule mwanao hatakubalika na hivyo atasimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

### B: KARO (ADA YA SHULE)

Ada ya shule ni Tsh. **35,000/=** kwa muhula kwa kila mwanafunzi. Ada hii ni muhimu na lazima ilipwe Benki, kwenye nambari ya akaunti **42501200023** NMB, jina la akaunti hii ni **Longido Secondary School.** Ni lazima mwanao aje na **Bank Pay in Slip** (nakala halisi ya risiti ya Benki).

NB: Kwenye **Bank Pay In Slip** ni muhimu kuandika majina ya mwanafunzi na kidato/darasa analoanza kusoma.

### C: 1. MICHANGO MINGINE YA SHULE:

i. Mchango wa Tahadhari ni Tshs. **5,000=**
ii. Mchango wa Taaluma ni Tshs. **30,000=**
iii. Mchango kwa ajili ya kuwalipa walinzi, wapishi, makarani, Matron na Wakutubi ni Tshs **30,000/=**.
iv. Mchango wa ukarabati wa majengo na samani za shule ni Tshs. **30,000**
v. **Kiti na dawati 20,000/=**

**Michango hii yote ilipwe kwenye Akaunti No. 42501200023 kwa kujaziwa Slip tofauti na Ada.**

C: 2 Michango yote katika kipengele hiki iletwe shuleni fedha taslimu (CASH), isilipwe benki.

i. Mchango wa nembo ya shule kwenye shati ni Tsh. **2,000=**
ii. Mchango wa picha na kitambulisho ni Tsh. **6,000=**
iii. Mchango wa huduma ya kwanza Tsh. **5,000=**
iv. Mchango wa bima ya afya **Tshs. 6000** kwa wasiokuwa na **Bima iliyoborshwa (CHIF) ni lazima**

**D: SARE YA SHULE**
Uvaaji wa sare ya shule ni lazima kwa kila mwanafunzi, hivyo mwanao awe na sare ya shule kama ifuatavyo:

**WAVULANA.**
i) Shati 2 nyeupe za mikono mifupi za aina ya tetroni na siyo mitumba.
ii) Suruali 2 rangi nyeusi, siyo mitumba, ziwe ndefu na zisizobana, ziwe na selebresheni (marinda) mbili, zenye mifuko ya pembeni kwa mshono wa "V" na mfuko wa nyuma mmoja. **(SURUALI ZINAZOBANA 'MODEL' HAZIRUHUSIWI KABISA).**
iii) Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2, viwe vya kufunga kwa kamba/gidamu, visivyo na kelele na visiwe vizito wala virefu kwa mbele.
iv) Soksi nyeusi fupi jozi 2 au zaidi.
v) Nguo za michezo: Raba, jezi rangi ya zambarau (purple) (bukta, tshert ) na tracksuit rangi ya zambarau)
vi) Suruali 2 za rangi ya blue bahari kwa ajili ya kushindia mara baada ya masomo kwa kuwa nguo za nyumbani hazirihusiwi.
vii) fagio 2 za chelewa, fagio 1 ya kukaushia maji (skwiza), ufagio laini 1(soft broom) na panga moja.
viii) Sweta rangi ya dark blue (bluu nyeusi) na tai yenye mistari rangi nyeusi na nyeupe.
ix) Taulo la kuogea.
**NB**: Usipopata sweta na tai vinapatikana maeneo ya jirani na shule kwa bei ya **Tshs. 20,000/=**

**WASICHANA**
i) Sketi 2 nyeusi, ziwe nzito na zenye marinda mengi, ziwe ndefu zinazofika katikati ya mguu toka kwenye goti hadi kwenye unyayo.
ii) Shati 2 nyeupe za mikono mifupi.
iii) Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2, vya kufunga kwa kamba/gidamu (siyo simple shoes), visivyo na kelele na visiwe vizito wala virefu kwa mbele.
iv) Soksi ndefu nyeupe jozi 2 au zaidi.
v) Nguo za michezo: Raba, jezi rangi ya zambarau (purple) track suit ya zambarau na fulana ya zambarau
vi) Gauni 2 za rangi ya bluu bahari zenye mikono mifupi na zenye makunjo/marinda, kwa ajili ya kushindia mara baada ya masomo kwa kuwa nguo za nyumbani haziruhusiwi (kitambaa kizito kama cha sketi ya shule)
vii) Fagio ngumu (hard broom) jembe moja lenye mpini.
viii) Kwa Waislamu, mfano wa Hijab iliyochaguliwa kutumika kwa wanafunzi wa kike imeambatanishwa (hijabu nyeupe na nyeusi tu)
viii) Sweta rangi ya dark blue (blue nyeusi) na tai yenye mistari rangi nyeusi na nyeupe (si ya kushona)
xi) Kanga vipande viwili na taulo kwa ajili ya kuogea.
**NB**: Usipopata sweta na tai vinapatikana maeneo ya jirani na shule kwa bei ya **Tshs. 20,000/=**



**LAZIMA KWA WOTE**
Mwanao aje na yafuatayo:-

1. Fedha Tshs. **15,000/=** kwa ajili ya kununulia T-sheti yenye nembo ya shule.
2. Bunda moja la karatasi zisizo na mistari (A4 Ream paper).
3. Vyombo vya chakula, bakuli, kijiko, kikombe na sahani visiwe vya plastiki, toilet papers (4).
4. Ndoo ya plastiki kwa ajili ya kuchotea maji yenye ujazo wa lita 10.
5. Vifaa vya darasani kama: Madaftari yasiyopungua 12 (makubwa), kalamu za wino bluu au nyeusi, penseli, Rula, Mathematical set na kamusi ya kiingereza na scientific calculator kwa mchepuo wa sayansi na uchumi na dissecting kit kwa wanafunzi wa biologia..
6. Godoro la Tanform,best au Dodoma (original) lenye ujazo sahihi na lenye upana na urefu wa 2½ x 4, lenye foronya ngumu. **<u>NB</u>: Zingatia vipimo vya godoro kwani ukija na vipimo tofauti halitapokelewa.**
7. Fomu Maalum ya kuthibitisha Afya yake (medical form) ambayo imeambatanishwa katika fomu hii, fomu hiyo ijazwe na daktari na iwasilishwe shuleni pindi atakapowasili. (TATIZO SUGU LIWEKWE BAYANA MWANAFUNZI APIMWE)
8. Blanketi nzito rangi yoyote kwa ajili ya kujikinga wakati wa baridi na mashuka mawili ya rangi ya **bluu bahari** (Usipopata mashuka yanapatikana maeneo ya jirani na shule kwa Tshs. 8,000/=.
9. Sweta ya rangi ya bluu bahari kwa ajili ya kushindia baada ya vipindi darasani. (usipopata sweta rangi ya bluu bahari yanapatikana maeneo jirani na shule kwa shilingi elfu 15,000/=).
10. T-sheti za bluu masai mbili nzito zisizo na maandishi yoyote kwa ajili ya kushindia baada ya vipindi darasani zenye kola si duara
11. Sanduku gumu la bati kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake muhimu (TRANKA)
12. Fedha za matumizi binafsi.
13. Saa ya mkononi na tochi isiyotumia umeme lazima kwa wote
14. Faili la kuwekea kumbukumbu za mitihani ya ndani.
15. Picha nne (4) mwanafunzi passport size, awe amevaa shati jeupe.

**NB: Ni marufuku mwanafunzi kufika shuleni na vitu vifuatavyo:-**

1. Nguo za nyumbani au kofia aina yoyote.
2. Vyakula vya aina yoyote mfano mkate, pipi, biskuti, sukari n.k
3. Vipodozi vya aina yoyote kama vile perfume, wanja, lipbam, rangi za kucha n.k
4. Redio, simu za mkononi, kamera n.k atakayebainika na vifaa hivi atafukuzwa shule.

**MUHIMU KWA WOTE**

1. Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi unaruhusiwa kuja kumtembelea mwanao tarehe ............... siku ya Jumamosi kuanzia saa 3 asubuhi – 10 jioni,kwa lengo la kujua maendeleo yake kitaaluma na kinidhamu. **Tafadhali usije na vyakula vya aina yoyote** kama vile chips, maji, juisi n.k.
2. Ni muhimu kumpatia mwanao fedha za kutosha kujikimu au fedha za matumizi binafsi kama matibabu na dharura nyinginezo awapo shuleni. Kumbuka hudhurio moja tu la kumwona daktari pale anapokuwa mgonjwa siyo chini ya Tshs. **5,000/=** bila dawa.
3. Siku za kuripoti shuleni ni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa kabla ya saa kumi kamili jioni (yaani siku za kazi na muda wa kazi).
4. Mwanafunzi anayetoka nje ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara aje na tiketi ya gari endapo atafika nje ya muda uliopangwa.
5. kila mwanafunzi anatakiwa aje na vitabu vya masomo kulingana na Tahasusi anayosoma.

## SHERIA ZA SHULE

Tabia njema (Heshima/Utii/Adabu/Nidhamu/Ustaarabu/) ni ya lazima na inatiliwa mkazo hapa shuleni. Mwanafunzi mwenye tabia mbaya anaweza kukosa Elimu ya Sekondari au hata Elimu ya juu. Kila mwanafunzi anapaswa kufuata sheria/taratibu/kanuni zote za shule pia kuwatii Walimu, Watumishi wasio Walimu, kuheshimiana na wanafunzi wenzake pamoja na watu wengine.

## A: SHERIA ZA JUMLA.

1. Hairuhusiwi kunywa pombe au kuvuta sigara/kiko au kutumia madawa ya kulevya ya aina yoyote ile.
2. Hairuhusiwi kuwa na mahusiano ya kimapenzi kati ya wanafunzi au mtu yeyote.
3. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa kutoka kwa Mwalimu wa zamu. Aidha Mtumishi yeyote wa shule akikuona mtaani/mjini au mahali popote ana haki ya kukutaka uonyeshe ruhusa.
4. Ruhusa ya kulala nje ya shule kwa sababu maalum itatolewa na Mkuu wa Shule au Makamu wake tu.
5. Kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi za mikono zitakazotolewa kulingana na utaratibu uliotolewa
6. Matusi ya aina yoyote ya kuandika au kutamka au kutumia ishara hayaruhusiwi.
7. Mwanafunzi unapaswa kujali na kutunza mali zako/shule/mtu yeyote, kwa mfano kutunza taa za umeme, miundo mbinu ya maji, kuepuka kuchora kwenye kuta, kwani uharibifu wowote utakaojitokeza kwa uzembe wa mwanafunzi utagharamiwa na mwanafunzi mwenyewe.
8. Sare za shule(uniforms) lazima zivaliwe wakati wa masomo na wakati wa kuruhusiwa kutoka nje ya shule.
9. Kila mwanafunzi ajiepushe na vitendo vya wizi wa mali za wanafunzi wenzake/mali za shule/mtu yeyote.
10. Kila mwanafunzi azingatie usafi wa mwili, mavazi, madarasa, mabweni, ukumbi wa chakula, na usafi wa maeneo ya shule kulingana na mgawanyo uliopangwa.
11. Kila mwanafunzi ajiepushe na vitendo vya ugomvi wa maneno au kupigana,
12. Hairuhusiwi kuchelewa kufika shuleni wakati wa ukaguzi au kutoka likizo. Aidha mwanafunzi kama uliruhusiwa kwenda mjini au mtaani ni lazima kuzingatia muda wa kurudi ulioandikiwa kwenye ruhusa na ruhusa hiyo lazima irudishwe sehemu husika.
13. Mwanafunzi ni lazima kuonyesha tabia njema ukiwa ndani na nje ya shule kwani shule ina haki ya kukuadhibu ikiwa utaonyesha utovu wa nidhamu katika mazingira ya aina yoyote
14. Magazeti au picha zisizofaa hazitakiwi shuleni pia hairuhusiwi kuandika/kuchora ubaoni/ukutani.
15. Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na tabia njema dhidi ya wanafunzi wenzake na watu wengine.
16. Mwanafunzi haruhusiwi kwenda kwenye nyumba ya Mtumishi yeyote bila ruhusa.
17. Hairuhusiwi kutumia bwenini vyombo vya umeme kama vile Pasi/Heater/Birika/Redio/Simu ua kufanya ufundi wa aina yoyote ile kwenye miundo mbinu ya umeme (bwenini au darasani).
18. Hairuhusiwi kuvaa kofia labda kuwe na sababu maalum zilizothibitishwa na daktari.
19. Kila mwanafunzi kwa vyovyote vile ni lazima kuhudhuria vipindi vya dini kulingana na Dini yake na mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini bila ridhaa ya mzazi.
20. Kila mwanafunzi anapaswa kutii wito wa kengele kulingana na utaratibu wa shule
21. Ikiwa kuna sababu maalum ya mwanafunzi kuandika barua kwa idara moja wapo hapa shuleni, ni lazima barua hiyo aandikiwe kwa Mkuu wa shule kupitia idara husika.

22. Kila mwanafunzi ni lazima awe na utii kwa Walimu na Watumishi wasio walimu au Wakuu wengine kwani ubishi na ujeuri wa aina yoyote hauruhusiwi kabisa.
23. Kosa la kufeli mitihani litapelekea mwanafunzi kuondolewa shuleni.

## A: SHERIA ZA DARASANI

1. Darasani ni mahali pa kujifunzia, kelele za aina yoyote haziruhusiwi. Kila mwanafnzi anatakiwa kukaa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na mwalimu wa darasa
2. Mahudhurio darasani ni lazima kwa kila mwanafunzi wakati wa vipindi na muda mwingine wa kujisomea ambao umepangwa na shule. Mwanafunzi mtoro atafukuzwa shule.
3. Mwanafunzi haruhusiwi kukaa kwenye meza au kiti cha mwalimu
4. Kila mwanafunzi ni lazima afanye usafi wa darasa kulingana na ratiba iliyopo.
5. Hairuhusiwi kufanya kikao chochote darasani bila ya ruhusa ya mwalimu wa darasa au mamlaka nyingine.

## C: SHERIA ZA BWENINI

1. Bwenini ni mahali pa kulala na si mahali pa kupiga kelele. Mazungumzo ya bwenini yawe ya maana na siyo matusi au lugha mbaya.
2. Haitakiwi kuwasha moto bwenini, Usafi wa bwenini ni wajibu wa kila mwanafunzi anaeyeishi bweni husika.
3. Hairuhusiwi kufanya vikao vya aina yoyote ile kwenye mabweni bila ruhusa ya mwalimu mlezi wa bweni.
4. Mwanafunzi akiingia au kutokea dirishani atafukuzwa shule.
5. Muda wa darasani huruhusiwi kuwepo bwenini.

## D. SHERIA ZA UKUMBI WA CHAKULA.

1. Kila mwanafunzi afuate utaratibu uliowekwa wa matumizi ya ukumbi wa chakula
   Kwa mfano; i) Mpango wa usafi wa ukumbi wa chakula ii) Mpango wa kukaa wa ukumbi wa chakula
2. Wakati wa chakula kelele hazitakiwi na hairuhusiwi kuja na viatu vya kuogea (slippers)
3. Kila mwanafunzi anatakiwa awe na tabia nzuri ya mezani, umwagaji hovyo wa chakula haitakiwi.
4. Usafi lazima ufanywe mara baada ya kifungua kinywa, baada ya mlo wa mchana na mlo wa jioni.
5. Usafi wa ukumbi wa chakula ni wajibu wa wanafunzi wote.
6. Mwanafunzi hatakiwi kuingia jikoni bila ruhusa.
7. Muda wa kuchukua chakula hupaswi kuvaa ndala bwaloni.

## E. UTARATIBU WA ADHABU.

1. Mwanafunzi yeyote anayepewa adhabu lazima aifanye, ujeuri au ubishi wa aina yoyote utasababisha kuongezwa kwa adhabu hiyo. Kosa la kugomea adhabu linahesabiwa kuwa ni utovu wa nidhamu.
2. Mwalimu/Walimu watamwadhibu mwanafunzi yeyote anayekiuka sheria/taratibu/kanuni za shule au sheria/taratibu/kanuni zitakazokuwa zimewekwa na mwalimu wa zamu/mwalimu wa darasa/mwalimu mlezi wa bweni/mwalimu wa maeneo ya usafi ua mwalimu yeyote.
3. Mwanafunzi atapewa adhabu kulingana na kosa alilolifanya.
4. Mkuu wa shule anaweza kutoa adhabu kwa makosa makubwa kwa kumwadhibu mkosaji/kumsimamisha masomo kwa muda au kwa kupitia Bodi ya shule mwanafunzi anafukuzwa shule.

## F. TAHADHARI.

**Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule.**

i. Wizi

ii. Kutohudhuria masomo bila taaifa/utoro/kulala nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule.

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.

vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.

vii. Kufuga ndevu.

viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.

ix. Uvutaji wa sigara.

x. Uasherati, uhusiano wa kimapenzi(wa aina yoyote ile), kuoa au kuolewa.

xi. Kusababisha mimba, kupata mimba au kutoa mimba.

xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

xiii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

xiv. Kutembelea majumba ya starehe, nyumba za kulala wageni, pamoja na nyumba za watumishi.

xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

xvi. Kudharau Bendera ya Taifa.

xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k

xviii. Udanganyifu wa mitihani ya ndani.

Wako katika utumishi,

HEADMASTER
LONGIDO SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 8530 NAMANGA
ARUSHA

**D. G. TEMU**
**MKUU WA SHULE**

---

SEHEMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE KWA HERUFI KUBWA

1. (i) Jina la Mwanafunzi ..........................................................................................

   NB: Jina liwe lile lililotumika katika mtihani wa Taifa kidato cha nne.

   (ii) Jina la Shule uliyomaliza elimu ya kidato cha nne ................................................

   (iii) Tarehe ya kuzaliwa ........................ kijiji ........................... kata .....................

   Tarafa ....................... Wilaya ........................... ...Mkoa ................................

2. AFYA:

   (i) Taja magonjwa yoyote makubwa uliyowahi kuugua kama vile TB, POLIO, KIFAFA, UKIMWI n.k.......................................... (ii) Taja matatizo yoyote ya afya yako .....................................

3. JINA LA MZAZI

   (i) Baba ........................................ Hai/amefariki lini ....................................

   (ii) Mama ........................................ Hai/amefariki lini ....................................

4. **KAZI YA:**

(i)Baba ............................ Dini .................... dhehebu ..........................................

(ii)Mama .......................... Dini .................. dhehebu ......................................

(iii)Anwani ya mzazi/mlezi ..........................................................................................

(iv) Mwanafunzi anaishi na (weka alama V sehemu iliyo sahihi)

(a) Baba tu [ ] (b) Mama tu [ ] (c) Wazazi wote wawili [ ] (d) Mlezi [ ]

5. **MZAZI/MLEZI/TAASISI ITAKAYOGHARAMIKIA MAHITAJI YA SHULE:**

(i) Jina ......................................................................

(ii) Kazi yake ni ........................................................

(iii) Anuani ya mzazi/mlezi............................................

(iv) Namba yake ya simu ..............................................

(v) Uhusiano wake....................... Mf. Baba, Mama, Dada, Mjomba n.k.

(vi) Dini yake ............................ Dhehebu .................

**NB: Taja ndugu watatu ambao wanaweza kutoa msaada kwa haraka na picha (passport) zao kwenye ukurasa wa kwanza wa fowm hii na passport moja ya mwanafunzi.**

| SN | JINA KAMILI | KAZI | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |

6. **UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI:**

Mimi .......................................Kidato cha ......... Nimezisoma na kuzielewa sheria/taratibu/kanuni zote za shule na hivyo ninakubali kujiunga na Shule ya Sekondari Longido na ninaahidi kuwa nitafuata sheria/taratibu/kanuni zote za shule ili nitimize lengo la kuja shule kwa manufaa yangu, familia, jamii na taifa kwa ujumla. Endapo nitakwenda kinyume na sheria/taratibu /kanuni za shule nitakubali kuadhibiwa/kufukuzwa shule.

Saini ya Mwanfunzi .......................... Tarehe ....................

7. **SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI/MLEZI/TAASISI HUSIKA.**

Mimi.................................................ambaye ni .....................nathibitisha kuwa taarifa hizo hapo juu ni sahihi. Nimezisoma na kuzielewa sheria/taratibu/kanuni zote za shule na ninakubali mwanangu apewe adhabu/afukuzwe shule ikiwa atakiuka sheria/taratibu/kanuni za shule. Ninaahidi kushirikiana na Uongozi wa shule na Watumishi wote kuhakikisha mwanangu anakuwa na Nidhamu na Juhudi katika masomo, nitagharamia mahitaji yake ya shule ili kumjengea mazingira mazuri ya kusoma katika kipindi chote atakachokuwa shuleni.

Saini ya Mzazi/Mlezi .............................. Tarehe .................

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRIME MINISTER'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

(*To be completed by a Medical Officer in respect of both Form I and V entrants*)

Student's Full Name ……………………………………………………………………

Blood count (*red and white*) ……………………………………………………………………

Stool Examination ……………………………………………………………………

Urinalysis ……………………………………………………………………

Syphilis test ……………………………………………………………………

TB test ……………………………………………………………………

Eye test ……………………………………………………………………

Ears ……………………………………………………………………

Chest ……………………………………………………………………

Pregnancy test (*for girls*) ……………………………………………………………………

Abdomen ……………………………………………………………………

Spleen ……………………………………………………………………

Additional information, for example Physical defects, infections, chronic or family disease etc.

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………

I certify that the student mentioned above is Normal/Bear attention to him/her for pursuing further studies.

Designation ………………………………………

Station ………………………………………

Signature and Official stamp ……………………

Date ………………………………………